**Agosti 2016**

Rafiki wapendwa,

Mwezi huu nimwekuwa nikitafakari tabia na matendo makuu ya Mungu. Kwenye Zaburi 9 tunamuona Mfalme Daudi akizungumza kuhusu Mungu kama hakimu wetu waaminifu. Kwenye Zaburi Daudi anamtukuza Mungu kwa kumfunulia haki zake anapohukumu mataifa yenye uovu. Kisha anapoomba kwa ajili ya fursa mpya za kukumbuka rehema za Mungu, Daudi ana ujasiri kuhusu hukumu za Mungu kwa waovu na uhuru kwa wale wanaoonewa na kuteseka.

Daudi anamsihi Mungu aje upesi na kuonyesha uweza wake Mtakatifu na utawala kwa mataifa maovu. Kisha anaendelea kumuomba Mungu kuwa Mungu atayakumbuka mateso ya Daudi na maumivu yake na kumpa sababu nyingi zaidi za kumtukuza Bwana.

1 Nitamshukuru Bwana kwa moyo wangu wote;
Nitayasimulia matendo yako yote ya ajabu. 2 Nitafurahi na kukushangilia wewe;
Nitaliimbia jina lako, wewe uliye juu.

3 Kwa sababu adui zangu hurudi nyuma; Hujikwaa na kuangamia mbele zako. 4 Kwa maana
umenifanyia hukumu na haki. Umeketi kitini pa enzi ukihukumu kwa haki. 5 Umewakemea
mataifa; Na kumwangamiza mdhalimu; Umelifuta jina lao milele na milele.

13 WEWE, Bwana, unifadhili, Tazama mateso niteswayo na wanaonichukia; wewe uniinuaye katika
malango ya mauti, 14 ili nizisimulie sifa zako zote; Katika malango ya binti Sayuni nitaufurahia
wokovu wako. Zaburi 9:1–5, 13–14

Hata katikati ya mataifa na watu waovu, Daudi anakumbusha kuwa:

1) **Mungu ni ngome (mahali penye ulinzi) kwa wanaoonewa.**
2) **Hawaachi wanaomtafuta.**
3) **Hasahau kilio cha wanaoonewa.**

9 Bwana atakuwa ngome kwake aliyeonewa, Naam, ngome kwa nyakati za shida. 10 Nao wakujuao
jina lako wakutumaini wewe, maana wewe, Bwana hukuwaacha wakutafutao. 11 Mwimbieni
Bwana akaaye sayuni, Yatangazeni kati ya watu matendo yake. 12 Maana mlipiza kisasi cha
damu awakumbuka, hakukisahau kilio cha wanyonge.

Nasi tunaomwamini, tunaomjua tuliweke tumaini letu kwake na kuyapeleka maombi yetu kwa Bwana tukifahamu na kuamini leo kuwa anasikia vilio vyetu naye hatadharau vilio vya wanaoumia. Mungu ni hakimu wetu wa haki na Yesu ni mfalme wetu wa pekee. Leo tunaweza kuwa na matumaini!

Mungu akubariki,

Peggy Banks
Mkurugenzi wa Kimataifa wa Huduma
Project Hannah

**Shuhuda kutoka Albania:**

Kwa miaka mingi hatukuwa na kanisa kijijini kwetu. Tuliposikia habari ya vipindi vya redio, tulifurahi sana. Vipindi vyenu vya redio vimetusaidia kukua ndani ya Kristo. Nataka niwashukuru kwa ajili ya vipindi vya *Wanawake wa Matumaini.* Kwa kuvisikiliza, nimepata taarifa nyingi sana na nimejifunza namna ya kuwa karibu na Mungu. **Jorgjie**

Mimi ni kipofu tangu kuzaliwa na huwa navisikiliza vipindi vyenu. Huwa napenda sana kusikiliza vipindi vya *Wanawake wa Matumaini* kila siku ya jumamosi na Jumapili. Vipindi hivi vimenifundisha kuimarika katika Bwana. **Antigoni**

Mimi ni msikilizaji wa mara kwa mara wa vipindi vyenu. Vipindi vya *Wanawake wa Matumaini* huwa vinanitia sana moyo. Nimeamua kumfuata Yesu na ninataka nijue jinsi ya kuwahudumia wengine vizuri zaidi. Nina maisha magumu na nimeteseka kwa vurugu nyumbani. Lakini ndani ya kila tatizo nimemuona Kristo kwenye maisha yangu. Nimeelewa kuwa kwa kupitia shida hizi, Mungu hutufanya kuwa wapya. Roho Mtakatifu ananikumbusha mstari huu: “Uwe jasiri, umeushinda ulimwengu.” **Jeta**

Ninamshukuru Mungu kwa ajili ya vipindi vya *Wanawake wa Matumaini.* Nimejifunza vitu vingi ikiwemo kujitunza mimi na kuwahudumia watoto wangu. Siku moja niliwasikiliza mkizungumzia mafua. Taarifa nilizozipata zilikuwa muhimu sana. Sikuwa najua jinsi virusi vinavyotoka kwa mtoto mmoja kwenda kwa mwingine. Niliandika njia hizo na nimekuwa mwangalifu sana mtoto wangu mmoja akipata mafua. Sikujua kuwa watoto wanatakiwa kunywa vitu vingi vya majimaji wanapougua. Asante kwa ajili ya kila kitu. **Lumturi**

Mimba zangu mbili ziliharibika na ilikuwa vigumu sana kwangu kuamini kuwa Mungu angeweza kunipa mtoto. Siku moja rafiki yangu akanialika kwenda kanisani. Nikaendelea kwenda kanisani na kumuomba Mungu. Akanifanyia muujiza wa ajabu kwenye maisha yangu. Amenibariki kwa watoto wawili na ninatarajia kupata wa tatu. Ninamshukuru Mungu kwa ajli ya vipindi vya *Wanawake wa Matumaini*. Ni kipindi kizuri sana ambacho hakitufundishi dondoo muhimu tu, lakini kinatuliza mioyo yetu. Mungu awabariki sana! **Silvana**

Nilikulia kwenye familia illiyomkana Mungu. Niliolewa nikiwa na miaka 17. Tuliamua kwenda Ugiriki kutafuta kazi. Tuna watoto wawili. Baada ya muda, mume wangu alipata ajali na kufariki. Nikarudi Albania na kusikia habari za kanisa la Kikristo. Nikaanza kwenda kwenye kanisa hili pamoja na watoto wangu wawili. Nikamjua Mungu aliyenisaidia na kunipa nguvu za kuwalea watoto wangu. Maombi ninayoyasikia kwenye kalenda ya maombi kupitia kwenye redio pamoja na vipindi vya *Wanawake wa Matumaini* vimenipa nguvu. **Alma**

Asante sana kwa ajili ya vipindi vyenu vya redio. Huwa ninavisikiliza vipindi vyenu vya redio asubuhi. Mmenihimiza kuomba. Huwa naenda kanisani, na sasa najua kuwa Mungu anayasikiliza maombi. Siku moja nilikuwa namuombea bibi yangu. Alikuwa anaumwa na akapona. Madaktari wakasema hatafanyiwa upasuaji tena. Nilifurahi sana na kujua Mungu ameyajibu maombi yangu. Pia nimemuombea baba yangu. Alikuwa mlevi. Ninamshukuru Mungu kwa kuwa ameacha pombe. Mungu awabariki. **Stelina, 16**

Mimi ni mwanaume lakini naipenda sana kalenda yenu ya maombi. Masomo mnayogusia kwenye kalenda hii yanasaidia sana. Nimejifunza mambo mengi kuhusu hali za wanawake ulimwenguni. Kuna wakati nilisikia mambo ambayo sikuyaamini hasa mliposema kuwa wazazi huwauza watoto wao kwa ajili ya kupata mahari. Asante kwa ufahamu mliotupa. **Sofokli**

Ninaishi Marekani lakini naipenda sana kalenda yenu ya maombi ya Albania. Huwa nasikiliza kipindi cha maombi ya kalenda kwa njia ya mtandao, na ninabarikiwa kutokana na mahitaji yanayoombewa. Ninafurahi sana maana mnawaombea akina mama. Mimi ni mama wa watoto wawili na ninajua kuwa ni vigumu sana kuwahudumia watoto na kuwafundisha kwa njia iwapasayo, kwa hivyo asante sana kwa ajili ya maombi yenu. **Ori, Facebook**